## 4.2.2 Kiswahili Paper 2 (102/2)

1. (a)

(i) kutengwa na mazingira ya nyumbani
(ii) kudhulimiwa mali na jamaa za wazazi
(iii) ajira ya watoto - Duma kutumikishwa shambani
(iv) kudidimizwa katika ulanguzi wa dawa
(v) kusababishiwa uraibu wa dawa
(vi) wasiwasi - Duma akiwa mchanga kujazwa wasiwasi / woga
(vii) badala ya mwajiri kumwonea Duma imani, anamshutumu kwa kushikwa
(viii) kuhatarishiwa afya kwa kuhitajika kuzimeza dawa ili kuzisafirisha ughaibuni
(ix) kukatiziwa malezi - anatolewa nyumbani akiwa mchanga / kabla ya ubwabwa wa shingo kumtoka
(x) kuumbuliwa kwa moyo utu /kufanywa kuwa na moyo mgumu /usugu / ugumu wa moyo
(xi) kusababisha matumizi ya dawa shuleni.
(xii) kumfanya kuwa mvunja sheria / kumhusisha katika ufisadi.

5 x 1 = 5

(b)

(i) **Magonjwa** - wazazi wa Duma wanatumia pesa nyingi kwenye matibabu; wanamwacha mnyonge hivyo kuwa windo rahisi la uraibu na ulanguzi wa dawa.
(ii) **Uyatima** - Duma anakosa walezi hivyo kutoswa kwenye ulanguzi.
(iii) **Tamaa** - jamaa za Duma wanampoka mali kutokana na tamaa. Duma anaingilia ulanguzi wa dawa kwa sababu ya tamaa.
(iv) **Ufisadi** - maafisa wa usalama wanapokea hongo na kuendeleza ulanguzi wa dawa zaidi.
(v) **Uraibu wa dawa za kulevya** unamfanya Duma kutojidhibiti, anaendelea kuzitumia na kuzilangua kwa kupata nguvu mpya / msukumo.
(vi) **Utoto/umri mbichi** - unamfanya Duma kuwa windo Jepesi la mjomba Duma.
(vi) **Umaskini**
(vii) **Marafiki/walimu** - kumfunza Duma matumizi ya dawa.

4 x 1 = 4

(c)

(i) Duma anakubali kuziuza dawa shuleni na sokoni.
(ii) Duma anajaribisha kutumia dawa hadi kuwa mraibu sugu.
(iii) Badala ya kuwajibika kubadilika Duma anajiona kuwa mtendwa.
(iv) Anakubali kumeza dawa ili kuzisafirisha.
(v) Duma anahalalisha matendo yake, hivyo kutoyarekebisha.

For more visit: eazyarabic.com

(vi) Duma anawahonga polisi aachiliwe, hivyo kudidimia zaidi katika maovu.

(vii) Anashirikiana na mwajiri wake ili kuzua mbinu mpya za kuendeleza uhalifu; anakosa tahadhari na kuishia kukamatwa.

(viii) Hata anapojiwa na wazo la kubadilika hatuoni akilifuatilia; analiahirisha.

(ix) Tamaa inamfanya asingatuke kutoka kwenye uhalifu.

4 x 1 = 4

**Tanbihi**

Baadhi ya watahiniwa wanaweza kujadili pande zote mbili wakatoa baadhi ya hoja za kupinga kama vile:

(i) Duma anaingizwa kwenye biashara hii na watu waliomzidi ki-umri - mjomba Papa.

(ii) Kupokwa kwa mali kulimfanya kutafuta mbinu za kujikimu.

Hata hivyo, kwa vile swali linamhitaji kuthibitisha kauli hii, hoja za kuunga zichukue alama zaidi (alama 3), alama ya kupinga iwe moja (1).

(d)

(i) Wenye makini / waangalifu / walio macho kupambana na wahalifu

(ii) Ndizo zinazomwendeshea maisha / amekuwa mraibu sugu /ndizo zinazompa msukumo wa kuendelea na uhalifu.

2. (a)

(i) Suala la kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula linahitaji kushughulikiwa kwa dharura

(ii) Kila binadamu anahitaji kupata chakula chenye virutubishi.

(iii) Serikali inapambana na tatizo la chakula kwa kutoa misaada

(iv) Wakati wa kiangazi wahitaji hasa hufa kutokana na njaa

(v) Kiwango cha chini cha uzalishaji na uhifadhi wa chakula husababisha ukosefu wa chakula.

(vi) Ukosefu wa maji huzikumba sehemu kame kutokana na uhaba wa mvua.

(vii) Ukosefu wa mvua huzua hali ya utegemezi.

(viii) Wengine hula hata visivyostahili kuliwa.

(ix) Mbinu hasi za ukulima huathiri utoaji wa mazao.

(x) Wakulima wengine hupalilia mmomonyoko wa udongo kwa kulima kando ya mito, kulima eneo lilelile na kutopanda mimea inayozuia mmomonyoko wa udongo.

(xi) Baadhi ya wakulima kutopanda mimea inayostahimili ukame

(xii) Wafugaji kufuga mifugo wengi wasiostahimili ukame na kusababisha vifo

(xiii) Watu kutojua umuhimu wa lishe bora

8 x 1 = 8

mtiririko - 1

Jumla - 9

For more visit: eazyarabic.com

(b)

(i) Serikali imechimba visima na mabwawa katika sehemu kame ili kunyunyizia mashamba maji.

(ii) Wakulima kupanda mimea ya kuatika inayokomaa haraka ili kukabiliana na njaa.

(iii) Kufuga kuku wa kututumuliwa wanaoweza kuuzwa na kununua aina nyingine ya chakula.

(iv) Wakulima kuhimizwa kutumia njia za kisasa za uzalishaji na uhifadhi wa chakula.

(v) Wakulima wadogowadogo wakome kuuza vyakula vyao kiholela .

(vi) Wanaoishi kwenye vinamasi wavitunze na kuvitumia kwa njia endelevu.

(vii) Vijana washauriwe kushughulikia kilimo mashambani.

(viii) Waishio mijini watumie visehemu wanavyopata kuendeleza kilimo cha bustani.

5 x 1 = 5
mtiririko - 1
Jumla - 6
**Au 6 x 1 = 6**

4. (a)

(i) Silabi ni kipashio cha utamkaji ambacho hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti. **mf nda - ma** ; katika : ndama

(alama 2)

**Au**

Ni sauti moja au zaidi zinazotamkwa kama fungu moja la sauti / kama sauti moja.
Mf. o - a katika oa

2/0 - (alama 2)

(ii)

| | | |
|---|---|---|
| afya | enda | upwa |
| anza | anga | igwa |
| ibra | uzwa | |

1 x 1 = (alama 1)

(b) yu - kitenzi kishirikishi / kishirikishi kipungufu
anajaribu - kitenzi kisaidizi
kujinasua - kitenzi kikuu

3 x 1 = (alama 3)

(c) Mpira haukuchezeka kwa sababu ya mvua nyingi.

au

Mpira haukuchezwa na wachezaji kwa sababu ya mvua nyingi.

2/0 - (alama 2)

(d) Dobi atakuwa amewapigia watu nguo pasi. 2/0 - (alama 2)

(e) **Udhaifu** wa kazi zao **<u>ulifichuka</u>** **<u>kabla ya</u>** **<u>kusitishwa</u>** kwa mradi ule.

(Kumalizwa)
(Kukamilishwa)
(Kuhitimishwa)
(Kukomeshwa)

($\frac{1}{2}$ x 4 = alama 2)

(f) (i) Kirai ni fungu la maneno ambalo hudokeza maana lakini maana hiyo si kamili.

**au**

Kirai ni fungu la maneno ambalo huainishwa kwa kuzingatia neno lake kuu. Kwa mfano, nomino ndilo neno kuu la kirai nomino.

(ii) (a) na mafundi - kirai husishi/kirai kihusishi.

(alama 2)


(b) wenye ustadi mkubwa - kirai kivumishi / kirai vumishi

(alama 1)
2x $\frac{1}{2}$ = 1

(g) Kinga ni jambo au dawa ya kujiepusha na madhara.
Kinga ni kipande cha ukuni chenye moto.
Kukinga ni kutayarisha bindo, mkono au chombo ili kupokea kitu.

(1 x 2 = alama 2)

(h)




(8 x $\frac{1}{4}$ = alama 2)

For more visit: eazyarabic.com

(i) (i) Wakimbizi ndio wanatamani.
(ii) Watu wengine wanatamani.
(iii) Wakimbizi watarudi nyumbani kwa wakimbizi.
(iv) Watu wengine watarudi kwao (hao wengine).
(v) Watu wengine watarudi kwa wakimbizi.

(2 x 1 = alama 2)

(j) dh + kikwamizwa / kikwaruzo
+ ghuna
+ menoni

(2 x 1 = alama 2)

(k) Huyo mwenyewe hakuzingatia funzo la lishe bora.

$4 \text{ x } \frac{1}{2} = (\text{alama } 2)$

(l) Maana zifuatazo zijitokeze:
Gharama (i) jumla ya bei ya kufanyia jambo/pesa zinazohitajika kufanya jambo.

(ii) unalopoteza kwa kutozingatia maagizo.

Karama - kipawa kutoka kwa Mungu.

2 x 1 (alama 2)

(m) (i) Wanafunzi hawakuingia darasani wala hawakutoa vitabu wakaanza kusoma.
(ii) Wanafunzi hawakuingia darasani, wakatoa vitabu na kuanza kusoma.
(iii) Wanafunzi hawakuingia darasani na hawakutoa vitabu wakaanza kusoma.

2/0 - (alama 2)

(n) Nukta pacha
(i) Hutumiwa kutanguliza maneno halisi ya msemaji.
Mwalimu: Nawashauri msome kwa bidii.
Wanafunzi: Tunashukuru.
(ii) Hutumiwa kutanguliza maneno yaliyo kwenye orodha.
Alienda sokoni kununua: mapera, machungwa na papai.
(iii) Kutenga saa na dakika - saa 8 : 30
(iv) Kutenga shilingi na senti: Shilingi 10:50
(v) Kutenga sura na mstari, Yohana 8:30

2x1

(0) **<u>Wingu</u>** la nzige

(p) Medali - nishani
Mchuano - Kinyang'anyiro, mchezo, mashindano, shindano, pigano.
(2 x 1 = alama 2)

(q) (i) Furaha - 1 - 1 (alama 1)
(ii) Nyasi - U - Z1/ Z1 (alama 1)

**Tanbihi**

Kuna baadhi ya watahiniwa ambao huenda wakatumia uainishaji wa ngeli unaozingatia viambishi awali vya nomino. Hawa pia watuzwe ipasavyo. Kwa mfano:

(i) Furaha - N - N
(ii) Nyasi - U - N / U - NY / N

(r) Mf

(i) Wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi **licha ya** kukabiliwa na hatari.
(ii) **Pamoja na** hatari iliyowakabili, wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi.
(iii) **Minghairi ya** kukabiliwa na hatari, wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi.

Mifano mingine: hata baada ya, ilhali, lakini, bali, bighari ya, ila

(s) **Majani ya mti huo** yalikatiwa ng'ombe wote na wafugaji.
Yambwa (tendwa) (alama 2)

4. (a) Kaida ambazo zinadhibiti sifa za lugha katika mazungumzo haya ni:

(i) Mada - uwekezaji
(ii) Umri / uhusiano - anawazungumzia vijana
(iii) Utungo - ni hotuba / mazungumzo ya moja kwa moja / ushauri - nasaha/ mawaidha
(iv) Muktadha - ni muktadha au hali rasmi kwani anatakiwa kutoa mazungumzo hayo.

Hoja zifuatazo zizingatiwe:

(i) Lugha rasmi - kuhusu uwekezaji.

(ii) Mtindo wa hotuba / mazungumzo ya moja kwa moja na hadhira / ushauri / mawaidha.

(iii) Msamiati au istilahi za kibiashara - unaohusu uwekezaji, kama vile biashara, hisa, faida, gharama. n.k.

(iv) Anaweza kutumia misimu ya vijana inapostahili ili kujinasibisha zaidi nao / kufanikisha mawasiliano.

(v) Kuchanganya ndimi, kwa mfano, kutumia Kiingeraza na Kiswahili; au hata *sheng* kwa kuiwekea mipaka pia.

(vi) Matumizi ya sentensi ndefu-ni hotuba / ushauri.

(vii) Anaweza kuishirikisha hadhira kwa kuiuliza maswali ya balagha, au kuwataka kutoa maoni.

For more visit: eazyarabic.com

(viii) Lugha elekezi - inayoshauri kuhusu njia chanya za uwekezaji. Hapa matumizi ya kauli au sentensi agizi yatatawala.

(ix) Lugha sanifu / lahaja sanifu itawale kwa vile huu ni utungo rasmi.

(x) Lugha inayotumia kauli shawishi ili kuwaonyesha umuhimu wa kuwekeza badala ya kutegemea ajira.

5 x 1 = 5

(b) (i) Msamiati wa kidini - kwa mfano, Jalali, Mungu, alleluia, amina.

(ii) Lugha chakavu / lugha ya kale, kwa mfano, sama badala ya mbingu.

(iii) Kunukuu vifungu kutoka kwenye msahafu - Biblia au Kurani ili kuwaaminisha waumini.

(iv) Lugha yenye toni kali ya kutisha hasa unapohubiri ili kukashifu tendo hasi.

(v) Lugha inayohimiza / inayoshawishi kutenda mema

(vi) Matumizi ya mafumbo, kwa mfano mbazi

(vii) Kurudiwa kwa vifungu fulani, kwa mfano Sala ya Bwana, Neema ya Bwana Yesu, amin.

(viii) Matumizi ya kweli kinzani / matumizi ya fantasia. Kusawiri mambo ambayo hayawezekani katika maisha ya kawaida.

(ix) Lugha inayoibusha mhemko / jadhba. Mfano, Amina, Amina

(x) Majibizano; kwa mfano: "Bwana awe nanyi - awe pia nawe"
"Bwana asifiwe - Amina"

(xi) Matumizi ya vihisishi au nidaa kama vile 'Ee', - ili kuibua hisia mbalimbali

(xii) Lugha inayojaza matumaini ya maisha mema. Mfano, 'kabla hujazaliwa nilikujua.'

(xiii) Lugha inayomhimiza binadamu kuwa mtegemezi kwa Mungu, k.v.
"Msaada wangu unatoka kwa Mungu..."

(xiv) Lugha inayoyasawiri maisha ya binadamu kama yanayodhibitiwa na nguvu asizo na uwezo kwazo. Hana lolote la kufanya kuhusiana na maisha yake. Kwa mfano, "Hata ukahuzunika vipi huwezi kuongezea hata pima moja kwenye maisha yako."

(xv) Kuchanganya ndimi - hasa katika mahubiri.

(xvi) Mtumizi ya viziada - lugha kama vile ishara za mikono na uso, na miondoko ya mwili ili kuhuisha uhubiri.

(xvii) Lugha ya kushauri au kuelekeza. Kwa mfano, 'bisheni, nanyi mtafunguliwa.'

(xviii) Kutasfidi lugha ili kuondoa aibu. Kwa mfano, 'kujua mwanamke', badala ya kujamiiana.

5 x 1